Jarida la kifasihi

# NGURUMO MWANDISHI

Toleo La XII
Septemba - MMXXII




"...rafiki na mpenzi wangu ni vitabu."

## KITABU NA MIMI

Bi. Zamira Sanguti

## YALIYOMO

**TAHARIRI**— Kitabu na mimi—Uk 02

**MWANDISHI WETU**— Jane Davis— Uk 03

**NEW IN TOWN**— Maji Mandiga Chatimiza Mwaka Mmoja— Uk 04

Serikali Yazindua Tuzo ya Uandishi Bunifu — Uk 04

**PITIO LA VITABU**— Kijiji Kisicho na Makaburi— Uk 05

**MAKALA**— Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu— Uk 06 na 07

**RIWAYA:** Usiwe Muuaji— uk 08 na 09

**HADITHI FUPI:** Tabia— Uk 10

**ANA KWA ANA**: Zamira Sanguti (Mahusiano yake na Vitabu)—Uk 11

**RIWAYA:** Mpigambio—Uk 12 na 13

**MATANGAZO:** Uk 14

**NGURUMO YA MWANDISHI**

**MHARIRI: RICHARD MWAMBE**

**MSAIDIZI: REY STANLEY**

**WASILIANA NASI**

**0766 974 865 AU 0672 160 016**

**WhatsApp: +255 734 550 514**

## TAHARIRI: Kitabu na mimi…

Kwa wasomaji wetu,

Ni mwezi wa Septemba, tunakutana tena katika jarida letu maridhawa la Ngurumo ya Mwandishi Toleo la 12. tunamshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutufikisha hapa na leo hii ninachelea kusema kuwa jarida letu limefunga mwaka mmoja.

Haikuwa safari rahisi, milima, miteremko, kona kali na butu, vyote vilikuwa ni sehemu ya njia yetu kupitia. Leo hii, ndani ya mwaka mmoja tu tunaona kuwa wazo letu limeambukiza wengine na sasa tuna majarida pepe kama haya takribani mawili. Fasihi lazima ijitajirishe kwa yenyewe.

Fasihi haitakuwa na maana kama watu wawili watakosekana yaani fanani na hadhira. Fanani hawezi kuwa fanani kama hakuna hadhira; na hadhira haitakuwa hadhira kama hakuna fanani. Haya makundi mawili yanategemeana kwa karibu sana.

Kitabu na mimi, ni moja ya uhamasisho kwako mdau. Unakipa nafasi gani kitabu katika moyo na maisha yako?

Katika toleo hili tunamuona Bi. Zamira Sanguti akituambia yeye hana rafiki wala mpenzi zaidi ya kitabu. Anakipa kitabu nafasi kubwa katika maisha yake.

Amini usiamini, ukikipa kitabu nafasi kubwa katika maisha yako basi nacho kitakupa nafasi kubwa katika kilichomo ndani yake. Kitakukomboa, kitakufunza, kitakuongoza, kitakuinua. Hiyo ndiyo siri ya kitabu.

Mwandishi wa kitabu ana mengi ya kutuambia, kutufundisha, na kutuelekeza. Lakini ni vigumu kwake kutukasanya wote ili kutimiza azma yake hiyo, ndiyo maana anaandika na kututaka tununue na kusoma. Ukiona mtu anasoma vitabu mpaka mia kwa mwaka ujue tayari maisha yake ni kitabu na kitabu kimemuweka mahala ambapo hakutegemea.

Anza sasa, soma kitabu, soma kwa dhati. Kila muda wako wa ziada ambao hauna la muhimu kufanya, soma kitabu iwe cha riwaya, maarifa mengine, hata cha dini. We soma, yaani soma, utanishukuru baadae.

Mwisho nawaomba tukutane pale viwanja vya Chuo cha Posta, Kijitonyama kwenye maonesho ya kimataifa ya vitabu. Mimi nitakuwepo na ukitaka tuonane niandikie ***whatsapp binafsi 0766974865.*** tutakaa tuongee!

***Richard Mwambe, Man in the mirror..***

# MWANDISHI WETU: JANE DAVIS

**Kama ilivyo ada, leo katika safu yetu ya Mwandishi Wetu, tunamleta Jane Davis. Je wamjua?**



Naitwa Jane David Sabini Mwanizuwa. Jina langu la utunzi natumia Jane Davis.

Nilianza rasmi kuandika mwaka 2017 baada ya kukutana na mwandishi Zuberi Maruma ambaye aliugundua uwezo wangu baada ya kunipa zoezi la kuandika stori. Akanishauri nianze kuandika akanifungulia ukurasa, akaniunga kwenye makundi ya waandishi na kuniongoza kila hatua hadi nilipoweza kujiongoza mwenyewe.

Safari yangu katika uandishi imekuwa yenye changamoto nyingi sana. Sikuwahi kufahamu namna ya kuhifadhi kazi zangu hivyo nilijikuta nikipoteza kila kitu baada ya kuibiwa simu mara tatu. Namshukuru Mungu nilinyanyuka nikaanza upya.

Kitu kikubwa kilichonifanya kuwa mwandishi ni kuisemea Jamii isiyo na sauti, kama watoto. Kuifikishia ujumbe hadhira Kwa yale yanayoendelea ndani ya Jamii.

Mpaka sasa nimeandika Riwaya 10 nazo ni

Penzi La Kahaba,
Kasindi Muosha Huoshwa
Sologa Omile,
Chozi Langu Litafutwa Lini?,
Ni Suala La Mpito
Barua Kwa Mwalimu
Vijiwe Vya Mtandaoni
Majani Ya Boga
The Pretender
Usiwe Muuaji

Na hadithi nyingi fupifupi ambazo Kwa bahati mbaya zilipotea kwenye kifaa na kubaki na mbili tu.

Hadi Sasa sijafanikiwa kuchapisha kitabu kutokana na gharama ila niko mbioni Inshallah nikijaliwa nitachapa kitabu chenye jina HAYANA MWENYEJI.

Waandishi kama Emmanuel Kway, Kamanda Amata, Zuberi Maruma na mwanamama Laura Pettie wananii*spire* kwelikweli.

Ujumbe wangu kwa waandishi haswa chipukizi, ni kuwa, tupambane kufikia malengo yetu tusikate tamaa kwani kuna watu nyuma yetu wanaponywa na maandishi tunayoandika.

Naiomba Jamii itambue na kuthamini kazi za waandishi. Waandishi wanajitoa kutumia muda wao na kuumiza kichwa kuandika aidha kukupa burudani au kuelimisha isiwadidimize bali iwape sapoti.

**Penda kusoma vitabu**

**Faida za kusoma vitabu:**

- Msisimko wa Akili
- Kupunguza Msongo wa Mawazo
- Kuongeza Ujuzi wa mambo mbalimbali
- Kuongeza Msamiati
- Huboresha Uwezo wa Kukumbuka
- Hukupa Uwezo Mkubwa wa kuchambua na kufikiri
- Huboresha Mtazamo na Umakini

Kazi zangu zinapatika katika Group na page za facebook

Kwa Sasa naandika katika kurasa za Simulizi Club Facebook na Instagram.

Lakini pia napatikana WhatsApp 0657360750.

## MAJI MANDIGA CHATIMIZA MWAKA MMOJA

Na Mwandishi wetu

MAJI MANDIGA si jina geni kwa wapenzi wa vitabu nchini. Naweza kusema ni kati ya vitabu bora sana katika kizazi chetu. Mwingine anaweza akajiuliza ubora wake ni upi mbona cha kawaida tu?

Tanzania tuna waandishi wengi sana, na kati yao wengi wamefanya vizuri na kujinyakulia tuzo mbalimbali ndani na nje ya nchi. Hii inadhihirisha kwamba tunajua kuandika na tunaandika kweli.
Mohamme Hammie Rajab, mtoto wa kiume wa aliyekuwa mwandishi nguli wa riwaya nchini, Hayati Hammie Rajab (apumzike kwa amani) akishirikiana na mkewe kipenzi Bi. Mariam Mbano walikipa ubora unaostahili kitabu hiki. Hilo la kwanza!

Timu nzima, iliyokiandaa mpaka kuchapwa iliundwa na watu wenye weledi mkubwa. Kilihaririwa na Laura Pettie, kikasanifiwa kurasa na Hamis Kibari. Hata kilipotakiwa kuwa cha Kiingereza kikatafsiriwa na Richard Mabala. Na pale walipoamua kukifanya maalum kwa watoto basi mkono wa Marco Tibasima ukafanya kazi ya kuchora.

Nakala zaidi ya 30,000 zikasambazwa bure. Kilifika vijiji mbalimbali Tanzania. Na sasa kinasomwa UDOM na UDSM. Kitabu hiki kimeipeleka tanzania kwenye tuzo ya James Currey Prize for African Literature 2022, Quramo Writers' Prize 2022.

Maji Mandiga kimeitangaza fasihi ya Kitanzania kwa namna moja au nyingine. Na tunategemea mengi kutoka kwacho hivi karibuni.
Hii ndiyo maana nzima ya kuwa mwandishi, yaani kuwa na malengo. Hongera Maji Mandiga kwa kutimiza mwaka na mafanikio makubwa.

## SERIKALI YAZINDUA TUZO ZA UANDISHI BUNIFU

*Dar es salaam*

**HAYAWI HAYAWI, sasa yamekuwa! Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kupitia Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia imezindua Tuzo maalum kwa waandishi wa kazi bunifu za kifasihi.**

Tukio hilo lililosubiriwa kwa hamu kubwa na wadau wa sekta hiyo nchini sasa si ndoto tena bali uhalisia. Ikiwa ni ahadi mojawapo ambayo waziri mwenye zamana Mh. Adolf Mkenda aliitoa wakati wa tamasha kubwa la waandishi wa vitabu lilioandaliwa na Umoja wa Waandishi wa Riwaya wenye Dira, UWARIDI hapo mwezi Juni mwaka huu.

Kwa miaka mingi sana waandishi wa kazi bunifu wamekuwa kama yatima tangu kupoa kwa chombo kilichokuwa kikiwaunganisha cha UWAVITA mpaka wale waandishi wa riwaya walipoamua kuunda chombo kipya cha kuwaunganisha yaani UWARIDI.

Tuzo hiyo iliyopewa jina la mwasisi wa taifa la Tanzania na Rais wa awamu ya Kwanza Mwl. Julius Kambarage Nyerere itakuwa chachu kwa waandishi kuandika kazi zenye tija na zenye kuelimisha jamii moja kwa moja.

Pamoja na kuwa tuna lugha yetu ya Kiswahili, bado hakukuwa na kitu ambacho kingeunganisha mambo haya mawili muhimu, yaani uandishi bunifu na lugha ya Kiswahili.

Tuzo hiyo imepokelewa kwa mikono miwili na waandishi na wameishukuru serikali kwa kukumbuka. Fauka na hayo, wameiomba kuzingatia weledi katika mchakato mzima wa kutafuta washindi watakaojinyakulia donge nono na mengineyo yaliyoandaliwa.

Kwa msimu wa kwanza ni tanzu mbili tu zitakazoingia katika kinyang'anyiro hicho, nazo ni riwaya na ushairi.

Tunategemea Tuzo ya Mwalimu Nyerere ya uandishi bunifu kuwa moja ya njia ya kubidhaisha Kiswahili ndani na nje ya nchi.

Haya tarumbeta limepigwa, asiye na mwana aeleke jiwe.


Hongera serikali kwa hili.

Mungu ibariki Tanzania na watu wake.

RM

PITIO LA VITABU

# KITABU: KIJIJI KISICHO NA MAKABURI




www.richardmwambe.com JAMVI la SIMULIZI

**KIJIJI KISICHO NA MAKABURI ni kitabu cha riwaya kilichobeba masimulizi ya kusisimua. Kitabu hiki kilichoandikwa na Mtalaze Dikson, kimeteka hisia za wasomaji wengi sana. Wasomaji waliokisoma wanasemaje?**

Mariam Mbano:

KIJIJI KISICHO NA MAKABURI kinazungumzia changamoto ambazo zipo katika jamii lakini hazizungumzwi kwenye baadhi ya mazingira na ukijaribu kuzungumza unaonekana labda umepitwa na wakati, una imani potofu, unaongea mambo yasofahamika wala kuthibitika.

Yaliyompata mwalimu Dickson katika kitabu hiki yamewapata walimu wengi au watu mbalimbali, binafsi nishasikia story nyingi zinazofanana na mazingira haya kiasi cha kuwafanya walimu kukimbia makazi au kuacha kazi ,kupoteza morali ya kazi.

Jamii zetu zina mila ambazo kwa namna moja au nyingine zinakwamisha maendeleo ya mtu mmoja au mwingine lakini na wewe kuzikumbatia changamoto hizo hurudisha maendeleo binafsi nyuma

Kongole kwako mwandishi Mtalaze Dickson kitabu kina utajiri wa lugha, utajiri wa matukio, inaonyesha *research* ya kutosha imefanyika hongera sana kwako mwanzo mzuri, naamini utafanya hima kutuletea part 2 yake

Mwalimu Edigar Mwinuka

**Je? na Labda… za KIJIJI KISICHO NA MAKABURI**

Wakati wakiendelea na kozi ya Utangulizi Mwalimu wa Kiswahili wa Kidato cha Kwanza nimeamua kuwapa wanafunzi wangu changamoto ya kusoma Riwaya ya kaka Mtalaze Dickson darasani.

Usomaji huo utafanyika darasani wakati ambapo hakuna Mwalimu wala kazi yoyote maalumu waliyopewa kuifanya.

Kabla ya kuanza zoezi hilo la usomaji tulikuwa na chemshabongo ya JE? NA LABDA, na mazungumzo yetu yalikuwa kama ifuatavyo ;

**Mimi ;** Unapata maswali gani unapoambiwa kipo kijiji mahali fulani hakina kaburi hata moja?

**Mwanafunzi** : Hicho kijiji labda ni kipya kimeanza leo

**Wanafunzi :** (kicheko)

**Mimi :** Labda ni cha siku nyingi ila watu wa hapo hawafi

**Mwanafunzi :** Hakuna watu ambao hawafi

**Mimi :** Labda wapo kwenye hicho kijiji tu.

**Mwanafunzi :** Basi watakuwa mizimu sio watu.

**Mimi :** Labda wanakufa ila hawazikwi.

**Wanafunzi :** Sasa wanaenda wapi?

**Mimi :** Sijui! nyie mnahisije?

**Mwanafunzi :** Labda wanapotea

**Mwanafunzi :** Wanapotelea wapi?

**Wanafunzi :** Kimya

**Mwanafunzi :** Labda hicho kijiji hakina watu

**Mimi :** Kijiji ni eneo lenye watu, eneo likikosa watu wanaoishi hapo sio kijiji.

**Mwanafunzi :** Basi mwalimu si tusome tu tujue kwanini tuandikie mate?

**Mimi :** Basi sawa hakuna haja ya kuandikia *wino* wakati *mate* yamejaa mdomoni

Chukueni vitabu tusome.

Mwandishi Mtalaze Dikson, anafanikiwa sana kuiteka hadhira kwa jina la kitabu hiki **'Kijiji Kisicho na Makaburi'** kila anayekutana nacho anajikuta ana hamu ya kujua ni Kijiji gani hiko? Kulikoni kisiwe na makaburi?

Kama hujawahi kukisoma basi bado nafasi unayo kwani kinapatikana katika maduka ya vitabu nchini.

## MAKALA: TUZO YA KITAIFA YA MWALIMU NYERERE YA UANDISHI BUNIFU

**Tafakari ya Mwafrika**



**©Na Mwafrika Merinyo**

Tangazo la Waziri wa Elimu na Mafunzo Stadi kuhusu serikali kutoa tuzo ya kitaifa ya uandishi bunifu kwa waandishi / vitabu bora ni jambo la kufurahisha na la kufurahiwa na jamii ya waandishi na Watanzania kwa ujumla.

Tangazo hili limeonyesha nia njema kwa upande wa serikali katika kuboresha elimu kwa kuchochea uandishi bora na usomaji katika shule za ngazi zote na vyuo hadi vyuo vya juu nchini.
Binafsi kama mwandishi ambaye natambua hamu ya mbunifu kuona kile anachokibuni kinanufaisha jamii nimefurahia sana hatua hii. Kwa nia hii pekee kama ilivyooneshwa katika tangazo husika, napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Dk. Adolf Mkenda.

Nia njema mara nyingi huhitaji kuambatana na/au kusaidizana na mkakati bora na mipango murua. Nalenga kusema kwamba jambo hili la tuzo linapaswa kutazamwa kwa umakini na kutekelezwa kwa weledi ili liwe na tija tarajiwa katika taifa.

Tuzo hii itakuwa alama kubwa katika taifa letu kama itatekelezwa kwa ufanisi. Itakuwa mara ya kwanza kuwa na tuzo ya kiwango cha kitaifa kwa waandishi bunifu inayoambatana na mambo matatu makubwa: utaifa, jina la mpenzi mkuu wa elimu na rais mstaafu (Mwalimu Nyerere) na kifuta jasho au zawadi ya fedha taslimu juu ya mrabaha atakaolipwa mwandishi kazi yake itakapochapwa kwa matumizi shuleni na vyuoni. Ni jambo la kihistoria.

DHANA NA UMUHIMU WA TUZO
Kumekuwa na kawaida ya utoaji tuzo katika tasnia na fani mbalimbali mahali pengi duniani. Baadhi ya tuzo kubwa na maarufu ni kama Tuzo za Nobel katika nyanja mbalimbali, Tuzo za Oscar, Tuzo za Grammy, Tuzo za Cannes na kadhalika. Sababu kubwa za utoaji tuzo ni pamoja na ukuzaji wa fani, kukuza ushindani katika fani, uhamasishaji weledi na ubora na utambuaji wa michango ya wanajamii katika maeneo muhimu katika jamii zao au hata jamii za kimataifa.

Hivi nadiriki kusema kwamba utoaji tuzo si jambo lililoshamiri sana katika nchi yetu. Zipo taasisi au asasi chache ambazo zimejipambanua katika kutoa tuzo, lakini tuzo hizi aghalabu zimegubikwa na malalamiko kutoka kwa wadau yahusuyo ukosefu wa uwazi, uwepo wa upendeleo, vigezo vyenye utata na uchapwa wa tuzo zenyewe, kwa maana ya kukosekana uzito au hadhi stahiki katika kile anachotunukiwa mhusika.
Kwa hoja hizo, nimeona kuna masuala kadhaa ambayo ingefaa yapatiwe ushauri na kuingizwa katika mkakati wa uandaaji na utoaji wa tuzo hii kubwa na ya kitaifa ya uandishi bunifu.

**UAMINIFU NA KUAMINIWA KWA WATENDAJI KATIKA KAMATI YA UTEKELEZAJI**
Naamini kwamba Mheshimiwa Waziri na timu yake ya ushauri au watendaji ni watu wenye heshima na ni watumishi wa kuaminiwa. Kwa msingi huo huo, kamati itakayoteuliwa kushughulikia tuzo hii wanatarajiwa kupimika katika vigezo hivyo na viwango vyao vya weledi katika fani husika, yaani uandishi bunifu. Watatakiwa wawe wambuji katika nyanja za ima utunzi, ufundishaji fasihi, uchambuzi, uhariri na/au uchapishaji. Aidha watendaji hawa hawataweza kufanya kazi bila wasaidizi wa kiofisi. Na hawa wasaidizi pia watatakiwa kufanya kazi kwa weledi na uzingativu wa usiri na uaminifu kama baadhi ya vipimo vya uhusika wao kwenye mradi wa tuzo. Mazingira haya ndiyo yatakayoweka

# TUZO YA KITAIFA YA MWALIMU NYERERE YA UANDISHI BUNIFU



Mh. Dkt. Adolf Mkenda

Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia

msingi mkuu wa kuaminika kwa jopo la utendaji na kuridhika kwa waandishi watakaoshirikisha kazi zao kwenye mchakato, lakini pia kwa umma utakaokuwa watumiaji wakuu au walaji wa mazao ya mchakato husika.

## UPEMBUZI YAKINIFU WA TANZU ANUAI ZA FASIHI NA VIGEZO VYAKE

Uandishi bunifu umegawanyika katika tanzu kadhaa, ikiwemo riwaya, mashairi, insha, hadithi fupi, tamthiliya na tenzi. Zaweza kuwepo tanzu zaidi ya hizi. Kamati ya tuzo itatakiwa kuandaa na kuwa na muongozo wa jumla wa tuzo na miongozo midogo na vigezo mahsusi kwa kila fani kwa msingi wa uwazi na ufafanuzi wa kiufundi ili washiriki wapate welewa usio na utata wowote watakapoamua kushirikisha kazi zao.

Katika yote haya, nadhani nia itakuwa kuhakikisha kwamba tuzo hii inakidhi ukuu wake, kwa maana ya utaifa na heshima kwa Mwalimu Nyerere ambaye alikuwa msomi, mwandishi mahiri na muasisi wa taifa letu.

## KURIDHISHA MAKUNDI MTAMBUKA

Nimeelezea kabla kwamba uandishi bunifu una tanzu kadhaa. Tuzo imetangazwa kama Tuzo ya Kitaifa ya Mwalimu Nyerere ya Uandishi Bunifu. Kwa msingi huu makundi anuai ya uandishi bunifu yanatakiwa yaonekane kutendewa haki sawa katika ushirikishwaji kwenye Tuzo. Sababu kubwa ni kwamba tanzu zote zina umuhimu wake katika fasihi na pia zinastahili kukuzwa katika usawa. Hii itahakikisha kwamba wasomaji, hususan wanafunzi na hadhira zingine za fasihi, wanapata wanachostahili bila kupunjwa kazi zitakazoshinda zitakapochapishwa.

Ni vema basi serikali, ambayo inaonekana ndio mdhamini mkuu wa tuzo hii (hizi?) kuhakikisha kwamba si waandishi wa riwaya, tamthiliya, mashairi, tenzi, insha, hadithi fupi wala bunilizi watakaolalamika kuwa wameachwa kando katika mpango wa tuzo. Haipaswi mdhamini kuonyesha upendeleo kwa fani moja juu ya nyingine, kwani tayari atakuwa amejijengea kukosa kuaminiwa katika hatua ya kwanza.

Ninaitakia Wizara, kamati itakayoteuliwa kusimamia Tuzo hii na washiriki watarajiwa kila la heri.

> Nalenga kusema kwamba jambo hili la tuzo linapaswa kutazamwa kwa umakini na kutekelezwa kwa weledi ili liwe na tija tarajiwa katika taifa.

Kazi iendelee!
Mungu ibariki Tanzania!

# HADITHI: USIWE MUUAJI—05



*Na Jane Davis*

*Ilipoishia…*

**Alichokiwaza ndicho kilichokuwa, vichupa vya mafuta havikuwepo mezani hapo.Alibinua meza kuangalia labda huwenda vimeangukia chini lakini hakuona kitu.Aliinama chini ya uvungu wa kitanda kutizama lakini kulikuwa patupu.**

*Endelea*

"Shemeji! Uliingia humu Leo?"Aliamwita shemeji yake akamuuliza.

"Hapana shem si ulikuwemo wewe" alijibu mke wa Masanja.

"Hakuna mwingine aliyeingia humu tulipoondoka?" aliuliza Masunga.

"Hakuna, hajaja mtu shem, kwani kuna nini?"

"Hamna kitu, kaandae uji wa mgonjwa" alijibu Masunga akiwa amechanganyikiwa.

"Dah! Chupa za mafuta zimeenda wapi?" akawaza akiwa kasimama wima jasho likimtoka.

Masunga alichanganyikiwa sana kwa kitendo cha mafuta hayo kupotea mule chumbani ilhali hakukuwa na mtu yoyote aliyeingia humo tofauti na yeye.

Hakuonesha wazi mfadhaiko wake wala hakumweleza chochote mama Masanja kuhusu upotevu wa mafuta. Alifahamu fika yule mama yuko katika wakati mgumu na anapambana na msongo mkubwa wa mawazo hivyo kumpa taarifa hiyo kungemuongezea matatizo.

Uji ulipokuwa tayari walisaidia kumpatia mgonjwa na mchana pia waliandaa viazi wakafanya kama siku iliyotangulia. Masunga alifurahi sana kuona mgonjwa chakula kinapita kwani wataalamu wa afya husema chakula ni dawa. Ikiwa mgonjwa anatumia dawa tu bila kula kupona kwake si rahisi kama yule anayepata dawa pamoja na chakula ambacho kinampatia nguvu mwilini.

***

"Nilikwambia shogaangu huyu kijana sio mtu mzuri kabisa lakini ukanibishia" aliongea Bi Stumai jioni ya siku hiyo alipofika kwa mama Masanja.

"Huyu kijana hana tatizo jirani mbona unamwandama namna hiyo" aliongea mama Masanja.

"Simwandami, hivi unafahamu nampenda sana mwanao Masanja na namchukulia kama mwanangu wa kuzaa, unatambua hilo?" aliongea yule mwanamke huku akijitikisa mwili wake.

"Natambua hilo lakini kwanini unamwandama huyu mwenzake?" alijibu mama Masanja.

"Mimi nafahamu ni kwanini simpendi huyu kijana mgeni" akasema

"Sawa lakini ni vyema ukaniweka wazi nami nikifahamu sababu kuu haswa inayokufanya umuone ni mtu mbaya?" aliuliza kwa udadisi Mama Masanja.

"Kama nilivyosema awali nampenda sana mwanao, hivyo ni jukumu langu kuhakikisha usalama wake. Siwezi kuona mtu anamtendea ubaya nikamwangalia na kufurahia" aliongea Stumai.

"Sasa nani kamtendea ubaya? unajua jirani sikuelewi kabisa, kila siku unazidi kunichanganya kwa habari zako mpya, ni juzi tu umekuja hapa ukaanza kumpiga picha mwanangu bila idhini yangu, kwa kweli sijapenda kabisa jambo hilo."

Hatimaye mama Masanja alitoa dukuduku lake lililokuwa likimkereketa moyoni.

"Heee! Hujapenda yaani mimi kumpenda mwanao namsaidia, hizo picha nimeenda kutafuta wadhamini mwanao akatibiwe nje leo unanisakama au unaniona najipendekeza sana" aliongea yule mwanamama kwa ukali.

"Sio hivyo jirani … kumpenda na kumtafutia wadhamini mwanangu ni jambo zuri lakini ulitakiwa uongee nami kwanza" Mama Masanja alishuka chini

akimtuliza bi Stumai ambaye tayari alikuwa kachukia.

"Sawa samahani sana nisamehe nimekoma mie ila nakutahadharisha tu kwamba muwe makini mnaishi na mtu hatari sana hamjui tu" aliongea bi Stumai kinafiki.

"Kwanini unasema hivyo?,ni mtu gani?" Mama Masanja akauliza kwa sauti ya upole

"Huyo huyo kijana unayemwamini na kumwachia akae na mgonjwa muda wote,"

"Bi Stumai naomba uwelewe basi huyo kijana ni mtu mzuri kabisa Hana tatizo jirani" alisisitiza mama Masanja.

"Hana tatizo! Ndivyo unavyojidanganya, kwa taarifa tu kijana huyo ni mshirikina," Bi Stumai akasema.

"Unasemaaa! Mshirikina! Bi Stumai mwogope Muumba wako, kwanini unamzushia kitu kama hicho huyu kijana?" Mama Masanja Aliuliza akiwa na mshangao.

"Nimzushie ili nipate nini sasa?Mimi nimemshuhudia leo kwa macho yangu mawili shahidi mdomo na pua" aliongea bi Stumai akibana sauti yake puani.

"Enhee hebu nielezee ulimshuhudia anafanya nini hadi umuite mtoto wa mwanamke mwenzako mshirikina?" Mama Masanja akauliza kimbea.

"Leo asubuhi kabla sijaenda dukani kwangu nilitaka kupita hapa kumuona mgonjwa. Nilipofika usawa wa dirishani huko nyuma mwili ukanisisimka. Nikawaza Kuna nini mbona kama taa ya hatari inawaka kichwani mwangu. Nikasimama hapo nikiwaza niendelee na safari au nirudi zangu nyumbani. Nikiwa natafakari mara akili ikanituma nichungulie pale dirishani nami bila kujiuliza mara mbili nikafanya hivyo. Hee shoga nilichokiona nilitamani kuzimia yaani sikuamini macho yangu," akasimulia

"Hee! Mbona unanitisha jirani uliona nini huko dirishani?" aliuliza Mama Masanja.

"Nimemshuhudia huyo kijana mgeni akimpaka dawa mwanao, yaani anamkanda kwa nguvu bila huruma aisee chozi lilinitoka bila kutarajia nilihisi uchungu mno" alijibu Bi. Stumai.

"Dawa gani hizo, Stumai uwe na uhakika na unachokiongea sio vizuri kumzushia mtu namna hiyo" aliongea mama Masanja.

"Madawa ya kienyeji na nina uhakika asilimia mia moja, naoña huniamini hebu tizama hiyo video nilimrekodi" akaongea huku akifungua pochi yake.
Bi Stumai alitoa simu yake akafungua upande wa video kisha akampatia simu hiyo. Mama Masanja akaanza kutizama video hiyo, video iliyokuwa ikimuonyesha Masunga akimfanyia masaji na kumpakaa mafuta rafiki yake Masanja ambaye ni mgonjwa.

"Mmh" alitoa mguno mama Masanja mara baada ya kumaliza kuitizama video Ile. Hakuguna Kwa sababu ya namna mwanae avyopakwa mafuta Bali hakuamini kama kweli mafuta hayo ni ushirikina kama anavyodai jirani yake bi Stumai.

"Mbona unaguna?"aliuliza Kwa dharau bi Stumai.

"Nashangaa tu hiki kinachoendelea" alijibu mama Masanja.

"Unashangaa eeeh! ndio hivyo endelea kushangaa hadi akuulie mwanao, madawa menyewe haya hapa" akatoa vichupa vidogo viwili vya mafuta kutoka kwenye pochi yake

"Hee! Umezipataje tena ilhali hujafika hapa leo?"Aliuliza Mama Masanja.

"Nilipomaliza kumrekodi nilijificha huko nyuma, na muda kidogo nikawaona mmetoka kwenda kuchota maji hapo ndipo nami nilipata nafasi nikaja nikanyatia taratibu nikaingia nikavibeba vichupa huyooo nikatoka kwenda dukani hata mkazamwana wako alikuwa huko jikoni na wala hakuniona" akasema bila hata chembe ya aibu usoni mwake.

"Khaaa! Wee mwanamke una hila hakika sikuwezi, Sasa kwanini uvibebe ikiwa waona ni ushirikina?" Mama Masanja akahoji, hakupenda hiyo tabia ya mtu kuingia ndani mwake kama chooni.

"Fumbuka wewe mwanamke lengo langu nije nikuonyeshe madawa anayopakwa mwanao, nadhani umeamini Sasa. Tunza hayo madawa kesho mapema takupitia twende kwa mtaalamu tumdhibiti huyu mchawi kabla hajawamaliza"aliongea Bi Stumai akaanza kupiga hatua kuondoka pale kwa mama Masanja.

***itaendelea***

# HADITHI FUPI: TABIA

## Na: Nelson Ntimba

***Ilipoishia...***

**Nilipoingia niligundua kuna milango miwili ya kutokea kwenye baa humo; wa kwanza ukiwa ni ule nilioingilia na wa pili ulikuwa upande wa ndani kabisa upande wa korido iloyo-elekea chooni.**

***Endelea...***

Bar yenyewe ilikuwa upande wa kushoto, ikiwa na viti, meza na ukumbi wa kucheza muziki. Halafu kwa mbele jukwaa ambapo wana-bendi walikuwa wanatumbuizia.

Bendi yenyewe ilionekana kama wamekutana kwa ajali tu. Kila mmoja alikuwa wa aina yake. Mtu wa Bass alikuwa ni mzee mmoja mweusi aliyekuwa amevalia suti na kaushi kwa ndani. Mpiga ngoma alionekana kama mjomba wake. Mwimbaji alikuwa ndiyo kituko. Alionekana mkubwa kuliko mpiga ngoma, ila mdogo kuliko mpiga Bass ingawa kiumbo aliwazidi wote.

Mpiga gitaa alikuwa tofauti sana. Alikuwa kijana mdogo tu. Na alikuwa ni mzungu. Umri wake kati ya miaka 20, na urefu kati ya futi 5 au 6. Alikuwa analicharaza gitaa lake haswaa.

Muziki ulikuwa mzuri, lazima nikiri hilo. Wale jamaa watatu weusi walikuwa wanajua kazi yao, na yule dogo mzungu pia alikuwa anajua wakati gani aguse nyuzi ipi kwenye gitaa lile. Yeye alikuwa amevaa tisheti nyekundu na suruali nyeusi na raba nyeupe. Uso wake ulionesha yuko kikazi muda wote. Hakuwa Mmarekani. Nilimkadiria angekuwa Mrusi, pia.

Nilitumia karibu nusu ya wimbo wao kuikagua baa yenyewe, kuhesabu watu waliokuwemo, na kusoma ishara za mwili za huyu na yule. Tabia za zamani hazipotei kirahisi. Kulikuwa na mabwana wawili wamekaa kwenye meza upande kwa upande huku mikono yao ikiwa chini ya meza. Bila shaka mmoja wao alikuwa anauza kitu fulani, na mwingine alikuwa ni mteja.

Wahudumu wa baa hii pia walikuwa wanamtapeli mmiliki wake kwa kuuza bia zao sana kuliko zile za bar. Walikuwa wanachukua mbili za baa na moja waliokuja nayo wenyewe pembeni. Mimi niliagiza bia moja na kwenda kukaa nayo kwenye kiti kilichokuwa ukutani na ni wakati huu ndipo nilipomuona yule binti akiwa peke yake kwenye meza, na mlinzi akiwa hayupo mbali naye. Nilikadiria pengine ile Mercedes Benz iliyokuwa pale nje ni ya kwao. Lazima alikuwa ni binti wa tajiri mmoja hivi. Sio bilionea. Ila milionea mmoja hivi aliyewekeza mtoto wake asome N.Y.U kwa miaka minne. Watu wawili tu wenye tofauti kati ya watu 80 waliokuwemo mule ndani. Sio tatizo hata.

Nilikuwa sahihi mpaka nilipoona jamaa fulani hivi wawili wengine.Walikuwa kama pea. Warefu na weupe. Warusi pia. Walikuwa wapo pamoja. Hakuna shaka kabisa. Inawezekana hawakuwa bora zaidi kuwahi kushuhudiwa na ulimwengu, lakini lazima nikiri hawakuwa wabovu sana pia.

Walikuwa wamekaa kivyao kwenye meza tofauti, lakini macho yao yalikuwa yapo kwa yule binti. Walikuwa na shauku, na nia fulani ingawa kulikuwa na uoga kidogo ndani yao. Nilielewa hali yao. Mimi pia nilikuwa nimeipitia mara nyingi. Kwahivyo nilijua hawa mabwana kuna jambo walikuwa wanataka kufanya.

Kwa akili zangu nilijua, kuna mamilionea wawili walikuwa na ugomvi, na mmoja kati yao alikuwa amemwekea mwanae mlinzi na dereva, na mwingine alikuwa anatuma watu kumteka huyo mwanae. Halafu ingekuja kuombwa hela, mateso na masharti mengine ili mtoto aachiwe. Biashara! Kwa staili kama ya Moscow. Lakini sio biashara yenye uhakika wa kufanikiwa sana. Utekaji nyara una kanuni nyingi na mara nyingi huwa unafeli kwa sababu zaidi ya milioni. Na kwa uzoefu wangu, urefu wa uhai wa mtu aliyetekwa nyara ni masaa 36 tu.

***Itaendelea toleo lijalo...***

# ZAMIRA SANGUTI: ... MAHUSIANO YAKE NA VITABU

**Na Richard Mwambe**

Mwezi huu wa Septemba, Ngurumo ya Mwandishi limefikia Dar es salaam, mpaka Kinondoni Morocco, Mtaa wa Nguchiro, Blok 43. Hapa kuna duka maarufu sana la kuuza vitabu kinajulikana kama Kona ya Riwaya.

Naingia hapa napokelewa na mwanadada mcheshi aliyejisitiri vyema na hijab hata unywele wake mmoja hauonekani.

Ni moja ya safari ndefu za jarida hili ambazo kwazo twakutana na wadau mbalimbali wa fasihi.

Nani asiyelijua hili duka, nje ya wapenzi wa vitabu vya riwaya waishio jijini Dar es salaam na miji ya kando yake?

Nimemkuta hapa ndani ya duka dogo lililosheheni mawazo lukuki na hadhimu yaliyowekwa kwenye vitabu. Nachelea kusema kwamba, huyu mwanadada mrembo na hivi vitabu wanafanana.

Nimejibanabana hapa dukani, sakafu na kuta za chumba hiki zimejaa vitabu, loh!

Kabla hata sijamwambia aseme nanyi, akaanza kunisimulia visa na mikasa kwa asilimia zaidi ya themanini ya vitabu vilivyopo humu ndani. Ana kipaji cha pekee!

Nimemkatisha hasiendelee kunisimulia ili aongee nanyi kidogo.

**Hebu tuambie wewe ni nani na maisha yako kwa kifupi...**

Mimi naitwa Zamira Sanguti ni mzaliwa wa Tanga. Kwenye familia yetu, mimi ni mtoto wa tatu kati ya watoto tisa.

Nilikuwa napenda sana kuwa mwanariadha, lakini baba yangu alikua hataki hata kusikia nacheza michezo hiyo. Kwa kuwa nilikua naongoza katika kikundi chetu nikawa namchukia sana baba.

Tofauti na mama, yeye alikuwa hana shida kwakuwa alikuwa mwalimu na alikuwa akinisapoti. Baba alipokuja kujua hivyo, akaenda hadi shule niliyokua nikisoma akawaambia kanipeleka pale nisome sio kukimbia kimbia. Basi, nikatolewa kwenye ule mchezo. kwakweli niliumia sana nikazidisha chuki kwa baba sitakuja kusahau




**Kwanini umejenga mahusiano makubwa na vitabu?**

Napenda kusoma vitabu kwanza mi sina rafiki, sina mpenzi. Rafiki na mpenzi wangu ni vitabu na nikikosa kitabu naumwa.

Hapa uliponikuta nauza vitabu, napenda kufanya kazi ya kuuza vitabu kwa sababu napenda vitabu..

**Waandishi wengi wanalalamika kuwa vitabu havina soko, wewe kama muuzaji unalizungumziaje hilo?**

Soko la vitabu ni kubwa hapa nchini kuliko mnavyofikiria. Watu wanapenda kusoma vitabu haswa mikoani.

Amini usiamini, wasomaji wengi wa vitabu ni wamama na wadada wanaobaki nyumbani. Kiukweli tunahitaji kazi mpya. Wandishi acheni uvivu

**Hebu waambie neno waandishi wakusikie, ongeza sauti wasikie vizuri**

Wandishi wa vitabu nawambia zipendeni kazi zenu na msiogope wa somaji pale wanapo taka kujua visa vya vitabu vyenu. Wengi wenu hampendi kuulizwa maswali tena mnachukia. Mimi mmojawapo, napenda kuwauliza maswali waandishi, lakini wengi wananichukia kwa kuwaulizauliza.

---

Kama upo nje ya Dar, Unaweza kuagiza kitabu na Zamira atakutumia bila wasiwasi. Ni mwaminifu sana. Basi wasiliana naye kwa 0655428085 (kwa ajili ya manunuzi ya vitabu tu!)

# MPIGA MBIO — 12

***Ilipoishia***

**"Yaani, pombe si chai, unaweza kubakwa hivi hivi!" Scogon akasema kwa uchungu. "Shida nini?"**

**"Pesa za yule Mmanyema!" Kebby akajibu.**

**"Mmanyema?"**

**"Ee Mzairwaa…"**

**"Kha! Zile milioni tano?" Scogon akauliza.**

***Endelea...***

"Hizohizo… wakati napambana na yule jamaa pale nje, nilimwona yule Mzairwaa… nikajua tumeisha!"

"Hah! Sijaikariri sura ya huyo askari, leo hii ningemweka kwenye kumi na nane zangu kama yule wa Moro'"

&&&&

Kama kuna siku ambayo Ikunda alijiona yuko peponi ni hiyo. Siku nzima aliendeshwa kwenye gari kama malkia. Duka hili alinunuliwa kile, na Duka lile alinunuliwa hiki. Shopping ilishika hatamu. Kenneth alimbadili mwanamke huyo kwa masaa machache sana. Tayari alimweka kwenye himaya yake na alimweka atakavyo.

Jioni hiyo alimpitisha saluni, akatengeneza nywele zake huku Kenny akimsubiri kwenye baa ya jirani. Alipomaliza wakatoka pamoja mpaka Star Light Cinema, wakaangalia filam moja iliyowakosha mioyo. Siku hii katika ukumbi huu ilioneshwa sinema ya Titanic. Hadithi ile ilimteka kabisa Ikunda akajikuta akipelekwa mbali kwa mawazo. Saa tatu usiku walitoka katika ule ukumbi wakiwa wameshikana mikono. Wakaingia garini tayari kwa safari.

"Sasa nakupeleka kwako!" Kenneth akamwambia Ikunda.

"Hata kwako ni sawa…" Ikunda akajibu na wote wakacheka na kugonga mikono yao. Kenneth alipogonga mkono wa mwanamke huyo akaudaka na kubaki na kile kiganja mkononi. Wakatazamana! "Nakupenda Ikunda!" akamwambia. Sauti ile ikatoka uvunguni mwa moyo wake kabisa. Ikunda alijisikia ganzi ikishuka kutoka utosini mpaka unyayoni.

Hili ndilo alilisubiri litamkwe. Ujumbe ule licha ya kusafirishwa kwa sauti, ulisafirishwa kwa hisia ya damu. Mikono ile iliposhikana bila kuachana, iliusafirisha ule ujumbe ndani kwa ndani. Ikunda akausikiliza masikioni na moyoni. Ukafika mpaka kwenye kiboksi kinachohifadhi itikio la upendo. Kiboksi ambacho Mungu amekiweka moyoni. Hakujibu kitu, alibaki akipumua kwa nguvu, kifua chake kilipanda juu na kushuka. Kenneth aliona matiti ya Ikunda yaliyojaa barabara. Yaliyosheheni mvuto. Yalivyokuwa yakipanda na kushuka, hali yake ilikuwa mbaya. Alihisi maeneo fulani ya mwili wake yakipata uhai. Macho yao yakatazamana. Ikunda akainama chini kwa aibu ya mapenzi na si aibu ya soni.

Gari likaondoshwa mpaka Tangi Bovu alipopanga mwanamke huyo.



Richard Mwambe

Mara hii hakuogopa kufika na mwanaume.

Wakafika mpaka sebuleni. Ilikuwa chumba—sebule, *self contain.* Samani za ndani zilikuwa za kawaida tu, na mapambo mbalimbali yalikipendezesha.

"Karibu ukae!" Ikunda akamkaribisha Kenneth.

"Asante... mapema sana. Nitakuja rasmi nile wali na samaki…" akajibu. Wakacheka. Kenneth akamkumbatia Ikunda. Miili yao ikagusana. Mtomaso wa upendo ukapenya miili yao.

"Asante kwa yote!" Ikunda akamwambia.

"Asante na wewe!" akajibu huku tayari akianza kuondoka baada ya kumaliza lile kumbatio. Kenneth alipoondoka, Ikunda akabaki peke yake. Ghafla akajikuta anaogopa kukaa peke yake chumbani! Lo!

&&&&

Asubuhi ya Siku iliyofuata ilimkuta Ikunda katika eneo lake la kazi kama ilivyo ada.

# MPIGA MBIO — 12



www.richardmwambe.com JAMVI la SIMULIZI

Ratiba haikubadilika isipokuwa tu yeye mwenyewe ndiye alionesha mabadiliko makubwa. Siku hii alionekana mwenye furaha sana, alifanya kazi kwa utulivu na tabasamu lisilokwisha. Muda na dakika ileile alikuwa kwenye kile kioo cha mbele. Akiwa anaendelea kusafisha, kwa mbali akamwona ampendaye akifanya mazoezi kama kawaida yake.

Ikunda akajisikia mwili ukimsisimka. Akaacha kufanya kazi na kutoka nje ili tu amwone vizuri. Naam! Ni yeye, yuleyule.

"Yaani unaacha kufanya kazi unakuja kumwangalia mwanaume!" sauti ya askari ikasikika kutoka kwenye kibanda wakitumiacho kwa mapumziko wakati wa lindo. Ikunda akageuka kutazama, Habib. Ikunda alihisi ganzi mwili mzima. Akamtazama kwa Jicho la chuki, "unanifatilia sana," akamwambia.

"Na ipo siku ntakupata tu… utaingia kwenye kumi na nane zangu!" Habib akamwambia Ikunda aliyekuwa bado kasimama hapo nje.

Habibu alimpenda sana Ikunda, lakini ndoano zote alizotupa hazikuweza kumvua samaki huyo. Kitendo kilichomtia hasira na uchungu hata akapanga mbinu za kumtenza nguvu binti huyo. Mkakati huo ulikuwa ukisukwa kichwani mwake peke yake. Hakutaka mtu yeyote ajue lolote. Aliamini kuwa mpango halifu ili ufanikiwe hutakiwi kushirikisha mtu. Alikuwa sahihi!

*Ipo siku yako, ntakuvuruga mpaka huyo mwanaume wako asikutake tena!* Akajisemea moyoni na kumaliza na sonyo refu. Habibu alijawa hinda moyoni hasa kuona mpita njia tu akichukua kile yeye kimnyimacho usingizi. Ikunda akajiondoa pale na kurudi ndani kuendelea na kazi, akiwaacha wale askari wakimsindikiza kwa macho.

"Vipi? Mbona mna mikwaruzano na mrembo?" askari mwingine akamuuliza Habibu.

"Huyu demu mshamba tu…"

"Kwani hujapata tu? Harakati zote zile!" yule askari akamwambia.

"Anajifanya mjanja kumbe hamna lolote. Huyo jamaa anayetroti-troti hapa nje si ndio anabeba mzigo!" Habibu akaeleza.

"Yupi? Huyu aliyepita sasa hivi hapa?"

"Huyohuyo! Na juzi walikuwa Mlimani City mzee kakumbatia goma dah! Iliniuma mzee… yaani vizawadi vyote vile demu ananitosa hivivi… hanijui kama mi Habib…"

"Utafanya yako kama kwa Tatu?"

"Habari ndo hiyo… kwanza sijui kwa nini wamerudisha hili lindo… na huyo jamaa anayempa jeuri ipo siku tutaumana!"

&&&&

Majira ya saa tano asubuhi, gari la Kebby liliegeshwa kando ya bahari huko Ununio. Kenneth akajivuta taratibu kuliendea, alijua swahiba zake wamefika kilichobaki ni kupanga madili ya pesa.

Aliuvuta mlango wa nyuma na kuingia. Gari lile likaondoka taratibu na kuchukua barabara ya kurudi mjini.

"Mna uhakika kila kitu ni sawa?" Kenneth akauliza.

"Yeah! Yule jamaa by saa saba atatoka pale!" Scogon akajibu huku Kebby akiendelea kupangua gia.

"Kila kitu kipo?" akauliza tena.

"Yeah!"

"Nipe changu," akamwambia Scogon. Kijana huyo akafungua kimkoba chake kidogo na kuchomoa bastola yenye ukubwa wa wastani. Akaitazama na kuifyatua magazini, imeshiba. Risasi nane zilikuwa kwenye vyumba vyake. Akatikisa kichwa juu chini na kuipachika kiunoni mwake.

"Asiumizwe mtu, labda kama ikibidi tu…" Kenneth akawaambia wenzake. Nao wakaitikia.

Vijana hawa watatu walishibana kwelikweli. Kila mmoja hakuwa na unasaba na mwenzake. Matendo yao, yaliyowafanya waingie jela ndiyo yaliyowakutanisha. Huko wakaunda urafiki, wakapanga mikakati ya kuishi pindi wakikutana uraiani.

***Itaendelea toleo lijalo***

**Tangazo**




www.richardmwambe.com
JAMVI la SIMULIZI

Jarida hili hutolewa na Jamvi la Simulizi kila mwezi
jamvilasimulizi@gmail.com